

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
ARISE AND SHINE MTHANI LA JARIBIO LA KWANZA-2020

102/1
KISWAHILI 102/1
INSHA
KARATASI YA KWANZA

MACHI/APRILI, 2020

1. Jibu

Insha iwe Tahariri

Iwe na tarehe

Iwe na utangulizi

Iwe na mwili/maelezo

Iwe na hitimisho-Jina la mhariri na wadhifa wake

Muundo/sura

(a). Pawe na kichwa cha gazeti pale juu nacho ni Gazeti la mwanzo mpya

(b). Pawe na kichwa-umuhimu wa vyama vya wanafunzi shuleni

(c). Utangulizi- uonyeshe lengo la kuandika ni kuonyesha umuhimu wa vyama vya wanafunzi shuleni

(d). Lugha ya mtahini ijikite katika uhalisi wa mambo shuleni-si porojo au uzushi

Adhabu ya sura

(i). Kukosa kichwa,kutotaja gazeti na kutojitambulisha na kadhalika ichukuliwe kuwa udhaifu wa kumtindo

(ii). Anayeaandika barua,kumbukumbu,na kadhalika ondoa 4s

Maudhui

- (a). Kukuza vipawa/talanta za Wanafunzi shuleni
- b). Kufunza uongozi shuleni-kila chama huwa na kiongozi
- c). Kuleta umoja na utangamano shuleni
- d). Kufunza uajibikaji miongoni mwa wanafunzi
- e). Njia za kujipatia riziki- chama cha wakulima chipukizi
- f) kuhifadhi mazingira-chama cha ulinzi wa mazingira
- g). Hukuza uzalendo kwa wanafunzi-chama cha maskauti
- h). Kukuza maswala ya kidini na kiroho-“ YCS’,”CU’
- i). Kuwatayarisha vijana kwa ulimwengu wa ushindani wanapomaliza shule
- j). Husaidia kukuza na kuhifadhi utamaduni-chama cha tamasha za muziki
- k). Njia ya kupalilia mtazamo changa kuhusu baadhi ya masomo kama vile chama cha Kiswahili.

2. Mtahiniwa aonyeshe hasara na faida, kasha, Atoe msimamo. Asipotoa msimamo,ni kosa la kimitindo

Akizungumzia upande mmoja pekee Asipite alama ya c+/10

Kuunga mkono

- Uhuru umesababisha utovu wa nidhamu
- Uhuru umewafanya vijana kujiingiza katika ulevi wa kupindukia,mavazi yasiyostahili na mengine
- Umewafanya vijana kutowatii-waalimu/wazazi wao.
- Uhuru umefanya vijana kutoamini utamaduni.
- Umewafanya vijana kujiingiza katika siasa sizizo na maana.
- Umewafanya vijana kuwa na maandamano ya kiholela na kuharibu mali

Kupinga

Vijana wanajieleza kikamilifu

[DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM](http://EcoleBooks.com)

Vijana wamechangia katika ujenzi wa taifa
Ukandamizaji umepunguzwa kwani wanaweza kujitetea
Sheria zinazowapa uhuru zimewafanya wazazi kuwajibika
Uhuru unafanya vijana kuingiliana na kufunzana mema

Tanbihi-mwanafunzi akadirie hoja zingine.

3.(a). Hii ni insha ya methali

(b). Kichwa kiwe methali husika –Andihakiye kovu hajaona jeraha

c). Maana-yoyote anayedharau kovu hujipata kuona jeraha au kidonda chenye. Tunaweza kukosa kuelewa kitendo kilivyokuwa na tukadharau matokeo yake.

(d). Matumizi-Tusidharau matokeo ya kitu au kitendo tusichokijua. Huenda kilikuwa ni muhimu

e). Mtahiniwa atunge kisa kinachoonyesha ukweli wa methali hii

(f). Mwanafunzi azingatie pande zote mbili za methali za kuzingatia ushauri wa upande wa kudharau ushauri ili maana ijitokeze

Tanbihi

Akishughulikia upande moja asipite alama 10 C+

4. Swali la nne

Msimulizi adhihirisha kuwa yuko katika eneo lingine geni ambako kuna hali ngumu. Kisa kinaweza kuonyesha mojawapo ya hali hizi

(i). Alitoroka katika eneo geni kwa ajili ya hali mbaya kwao. Pia huko ugenini kuna shida

(ii). Alihamia ugenini ili kutafuta ajira, elimu, matibabu au ndoa. Anapata hali ngumu. Kwa vyovyote vile, aliyotarajia msimulizi sio aliyopata

- Msimulizi atumie nafsi ya kwanza ili kisa kimrejeelee

- Akimrejelea mtu mwingine asiye msimulizi atakuwa amepotoka kimaudhui. Atuzwe D 03/02
- Endapo hataonyesha kuwa yuko katika eneo la kigeni asikofahamu,amejitungia swali. Atuzwe D-02/20. Iwapo hataonyesha hali ngumu lakini awe eneo geni,amepotoka . Atuzwe D. 03/20